*Mulika, Na. 41 (2), 192-205*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Fonolojia ya Nomino na Vitenzi katika Kimochi

*Clarah Nelson Moshi*[1]
Shule ya sekondari ya Kiboriloni - Moshi
&
*Joseph Hokororo Ismail*[2]
Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na41t2.5

**Ikisiri**

Makala haya yamelenga katika kufafanua vipengele anuwai vya fonolojia vipande sauti vya lugha ya Kimochi. Miongoni mwa vipengele vya kifonolojia vilivyoangaziwa ni irabu, konsonanti, muundo wa silabi, na michakato ya kifonolojia kwa kutumia nadharia ya vipande sauti Huru, iliyoasisiwa na Chomsky na Halle (1968). Data zilizotumika zimekusanywa uwandani katika vijiji viwili vya Mori na Mbokomu vilivyo katika wilaya ya Moshi vijijini, mkoa wa Kilimanjaro. Kama ilivyo katika lugha nyingi za Kibantu, imeonekana kwamba Kimochi kina jumla ya irabu tano (5) na konsonanti thelathini na moja (31) na kwamba michakato mbalimbali inayojitokeza katika Kimochi ni majumui. Hivyo makala haya yatasaidia kwa wanaisimu linganishi kuona mfanano wa vipengele vilivyoshughulikiwa humu na vile vinavyojitokeza katika lugha nyingine za kibantu.

## 1.0 Utangulizi

Kimochi ni lugha ya Kibantu inayozungumzwa na baadhi ya jamii ya Wachaga wa mkoa wa Kilimanjaro ulioko Kaskazini Mashariki mwa Tanzania Bara. Jamii ya Wachaga haina lugha moja ambayo inazungumzwa na wanajamii wote wanaoitwa Wachaga. Mkoa wa Kilimanjaro una jumla ya "lugha"[3] asili kumi na moja zinazotumika katika mawasiliano ndani ya jamii hiyo. Lugha hizo ni Kimasai, Chasu, Kigweno, Kirombo, Kimashami, Kivunjo, Kimochi, Kiuru, Kikahe, Kiwoso na Kisiha. Hii ni kwa mujibu wa Mradi wa Lugha za Tanzania (MLUTA, 2009). Katika lugha hizo kumi na moja, ukiondoa Kimasai, Chasu na Kigweno, lugha nane zinazobakia ni lugha za Kichaga.

Kwa mujibu wa MLUTA (2009), lugha ya Kimochi ina jumla ya wazungumzaji 36,823, wanaoishi katika miteremko ya Mlima Kilimanjaro katika wilaya ya Moshi Vijijini, katikati ya wilaya za Rombo na Hai. Wazungumzaji 10,321 wanaishi

[1] **Baruapepe:** clarahnelson08@yahoo.com na ismism3@gmail.com
[2] **Baruapepe**: jihokororo@yahoo.com
[3] Tunaziita "lugha" kwa sababu hadi sasa hakuna utafiti uliofanyika kuzibainisha kama ni lugha au lahaja.

Moshi mjini, kwa hiyo, jumla ya wazungumzaji wote wapatikanao Kilimanjaro ni 47,144. Eneo la asili la wazungumzaji wa Kimochi limepakana na Uru kwa upande wa Mashariki, upande wa Magharibi eneo la Kirua-Vunjo, upande wa Kaskazini eneo la uzio wa hifadhi ya Mlima Kilimanjaro na Kusini eneo la Kiboriloni lililoko Moshi mjini.

## 2.0 Vipengele vya Kifonolojia

Fonolojia ina vipengele ambavyo vinaangazia namna lugha inavyojibainisha katika umbonje kutokea katika umbondani la maneno yake. Katika makala haya tunaangazia vipengele vya kifonolojia vya irabu, konsonanti na viyeyusho, muundo wa silabi na michakato mbalimbali ya kifonolojia. Pia, tutaonesha tangamano la irabu, muungano wa sauti, mabadiliko ya sauti na udondoshaji wa sauti. Kwa sababu hakuna fonolojia katika ombwe, katika makala haya tutaona na kujifunza baadhi ya vipengele vya kimofolojia vinavyoathiriana na vipengele vya kifonolojia katika Kimochi.


## 2.1 Irabu katika Kimochi

Lugha ya Kimochi ina irabu fupi tano (5) ambazo ni /a/, /e/, /i/, /0/ na /u/ na irabu ndefu tano (5) ambazo ni /a:/, /e:/, /i:/, /o:/ na /u:/. Wakaa na mpangilio wa utokeaji wa irabu katika baadhi ya lugha, ikiwamo lugha ya Kimochi huwa na dhima yake. Katika Kimochi kuna utokezeaji wa irabu moja na irabu mbili. Utokezeaji wa irabu mbili unaweza kuwa irabu hizo zinafanana au zinatofautiana. Imeonekana kuwa katika Kimochi si kila mara mfuatano wa irabu mbili zinazofanana unapotokea katika neno ni irabu ndefu, bali wakati mwingine huweza kuwa ni irabu mbili tofauti au ni urefu wa ufidiaji (taz. Massamba 2005: 88-104). Kwa kuwa kipengele cha irabu ndefu, irabu mbili zinazofuatana na urefu wa ufidiaji ni mada pana, hatutaielezea kwa kina kwa sasa.

Nelson (2013) anaeleza kuwa katika Kimochi irabu zikiwa na toni tofauti basi ni irabu mbili tofauti hata kama zinafanana. Kwa mfano: ***kaátsa*** **–** “kawasha” katika kitenzi hiki irabu zilizopigiwa mstari chini ni irabu zinazofanya kazi tofauti. Irabu ya kwanza “***a***” ni sehemu ya silabi “***ka”*** ni silabi ya kiambishi awali kitangulizi chenye sifa ya njeo ya wakati uliopo kitambo kifupi kilichopita. Pia, irabu “***a***” ya pili ni silabi ya kwanza ya shina la kitenzi chenye silabi mbili ambacho ni ***atsa*** – “washa**”**. Vilevile, inaonekana kuwa kunapotokea mchakato wa udondoshaji au uyeyushaji, na ikatokea irabu mbili zilizofanana kuwa pamoja, inaweza kuwa ni irabu ndefu au ni irabu mbili tofauti. Kwa mfano, *naleéndo* “alietwa” toka katika *“nalehéndo”* baada ya kudondosha /h-/ ya shina la kitenzi, tunaona kuwa kunatokea irabu mbili tofauti. Irabu ya kwanza ni kilele cha silabi */-le-/* ya kiambishi cha njeo ya wakati uliopita hali timilifu. Irabu ya pili */-e-/* ni sehemu ya mzizi wa kitenzi /-end-/ cha shina */endo/* “letwa” kauli ya kutendwa.

Kimochi kina irabu ndefu kama inavyojitokeza katika vitenzi *ipéléétsa* "kukera" na kitenzi *idáá* "kunuka"; tunaona kwamba baadhi ya irabu ndefu zina J. Kwa kudokeza tu, irabu ndefu zinajitokeza pia katika baadhi ya nomino kama *ngóó* "moyo", *míí* "mume" na *máwee* "matiti". Irabu ndefu zinabeba ama J au C katika ama umoja au wingi na kuwa na kiimbotoni cha JJ au CC kutokana na usambaaji wa toni.

Tuangalie otografia katika Kielelezo Na. 1 cha mpangilio wa irabu Katika Kimochi:




***Kielelezo Na. 1: Mpangilio wa irabu za Kimochi***

Tunapoangalia kwa makini Kielelezo Na. 1, tunaona kwamba kati ya irabu (10) za Kimochi kuna zile za mbele juu /i/, /ii/; kati / ε /; na chini/εε/. Katika irabu ya nyuma, kuna irabu funge /u/ na /uu/, nusu wazi/ɔ/ na wazi /ɔ ɔ /. Pia kuna irabu kati za Kimochi ambazo ni /a/ na /a:/. Katika Jedwali Na. 1, tuangalie matumizi ya irabu hizi katika Kimochi kama ifuatavyo:

## Jedwali Na. 1: Otografia ya Irabu za Kimochi

| **Otografia** | **Herufi za Kifonetiki** | **Kimochi** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| /i/ | [i] | *Ionza* | kunyonyesha |
| /u/ | [u] | *Uhama* | kojoa |
| /e/ | [ε] | *engera* | ongeza |
| /o/ | [ɔ] | *oloka* | inuka/simama |
| /a/ | [a] | *Atsa* | washa |
| /ī/ | [i:] | *Iila* | kuchwa |
| /i/ | [i] | *Ila* | kutakata |
| /ū/ | [u:] | *Iruuwa* | kuloweka |
| /u/ | [u] | *Ruwa* | Mungu |
| /ē/ | [ε:] | *Ipeleetsa* | kukera |
| /e/ | [ε] | *ipeletsa* | kupekecha |
| /ō/ | [ɔ:] | *Ihoo* | hapo |
| /o/ | [ɔ] | *Iho* | jino/jiwe |
| /ā/ | [a:] | *Idea* | kunuka |
| /a/ | [a] | *Ida* | kupita |

**Chanzo:** Data za Uwandani (Machi, 2020)

## 2.2 Konsonanti katika Kimochi

Lugha ya Kimochi ina jumla ya konsonanti 31, ambapo kati yake konsonanti halisi ni (29) na viyeyusho viwili (2) ambavyo ni /j/ na /w/. Kwa kuzingatia vigezo vya mahali pa matamshi na namna ya matamshi, konsonati hizi zaweza kuoneshwa katika Jedwali Na. 2, kama ifuatavyo:

### Jedwali Na. 2: Konsonanti za Kimochi

| | | | **Mahali pa Matamshi** | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Midomo** | **Midomo meno** | **Meno** | **Ufizi** | **Kibinua Ulimi** | **Kaakaa gumu** | **Kaakaa laini** | **Koromeo** |
| **Namna ya matamshi** | Vipasuo | Si ghuna | p | | t̲ | t | | c | k | |
| | | Ghuna | b | | | d | | | g | |
| | | Mpumuo | $p^h$ | | | | | | | |
| | Vizuio-kwamizi | Si ghuna | | ɟ̶ | | ʦ | | | | |
| | | Ghuna | | | | | | ɟ̇ | | |
| | Kigonge / Kipigo | Si ghuna | | | | | ṛ | | | |
| | | Ghuna | | | | | ḍ | | | |
| | Vikwamizi | Si ghuna | | f | | s | | š | | |
| | | Ghuna | ß | v | | z | | | | h |
| | Nazali | | m, ṁ | | | n, ṅ | | ɲ | Ŋ | |
| | Andamio Nazali | | mb | ɱ, mf | ndz | nd | | nɟ | ŋg | |
| | Viondoshi | | | | | | | k’, l’ | ṅŋ’ | |
| | Vilainisho | | | | | r | ł | l | | |
| | Viyeyusho | | w | | | | | j | | |

Konsonanti hizi zinaweza kutumika katika maneno ya Kimochi kama inavyojionesha katika jedwali 3, otografia ya Konsonanti katika Kimochi:

### Jedwali Na. 3: Otografia ya Konsonanti katika Kimochi

| **Herufi za Kifonetiki** | **Otografia** | **Kimochi** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| [p] | /p/ | *ikapo* *[ikápo]* | kupigwa |
| [$p^h$] | /$p^{h}$/ | *$p^h$usuo* *[$p^h$usúo]* | mwaga |

| | | | |
|---|---|---|---|
| [t̠] | /t̠/ | *it̠ema*<br>*[it̠éma]* | kucheza |
| [t] | /t/ | *iterewa*<br>*[iteréwa]* | kuomba |
| [d] | /d/ | *kyadaa*<br>*[kjadáa]* | kimenuka |
| [c] | /ch/ | *ngaicho*<br>*[nŋaíco]* | nimesikia |
| [k] | /k/ | *iseka*<br>*[iséka]* | kucheka |
| [ŋ] | /ng/ | *songuo*<br>*[sonŋúwo]* | tangulia |
| [ß] | /bh/ | *yave*<br>*[jaße]* | yawe (mungu) |
| [ ɟ] | /pf/ | *ipfa*<br>*[íɟa]* | kufa |
| [ʦ] | /ts/ | *isetsa*<br>*[isétsa]* | kuchekesha |
| [nɟ] | /nj/ | *ifunja*<br>*[ifúnɟa]* | kuvunja |
| [ṛ] | /r̠/ | *ir̠aa*<br>*[íṛaa]* | kuvaa |
| [ḍ] | /d̠/ | *lud̠ed̠e*<br>*[luḍéḍe]* | tuongee |
| [f] | /f/ | *fosia*<br>*[fosía]* | umekwisha |
| [s] | /s/ | *isonguo*<br>*[isonŋúo]* | kutangulia |
| [nz] | /nz/ | *inonza*<br>*[inónza]* | kumwagilia |
| [š] | /sh/ | *sheringa*<br>*[šerínŋa]* | vyakulinda |
| [ndz] | /ndz/ | *iondza*<br>*[ióndza]* | kunyonyesha |
| [h] | /h/ | *hendeny*<br>*[hendéɲ]* | nendeni |
| [m] | /m/ | *mukundane*<br>*[mukundáne]* | mpendane |
| [mb] | /mb/ | *isember̠a*<br>*[isembér̠a]* | kusogeza |
| [ɱ] | /mv/ | *fumvuhu*<br>*[fumvúhu]* | mlimani |

| | | | |
|---|---|---|---|
| [n] | /n/ | *inandza* *[inándza]* | kulewesha |
| [ň] | /ny/ | *inyamar̲a* *[iɲamár̲a]* | kuharibu |
| [ŋ] | /ng'/ | *ing'ana* *[iŋána]* | kukuwa |
| [r] | /r/ | *imtarama* *[imtaráma]* | kumsaidia |
| [ɬ] | /l̲/ | *ikel̲er̲io* *[ikeɬer̲ío]* | kusubirishiwa |
| [l] | /l/ | *ilaa* *[iláa]* | kulala |
| [w] | /w/ | *iwaha* *[iwáha]* | kuua |
| [j] | /y/ | *komkoya* *[komkója]* | ukimkuta |

**Chanzo:** Data za Uwandani (Machi, 2020)

Pia, katika Jedwali Na. 3 tunaona kwamba miongoni mwa konsonanti hizo kuna nazali [ṁ] na [ṅ] zinazotamkwa kama nazali mbili ambatani, yaani /mm/ na /nn/ kama inavyoonekana katika Data Na.1:

(1)

a) */ṁbá/ → [mmba*] "nyumba"
b) */ṅdá/ → [nnda]* "shamba"
c) */ṅdé/ → [nnde]* "twende",
d) */ṁbé/ → [mmbe*] "ng'ombe"
e) */ṁbesé/ → [mmbese*] "muulize"

Katika (1), maneno yaliyo na andamio nazali yanaonekana kuwa mfuatano wa sauti nazali ambao uko katika umbo la ndani la silabi husika na kufanya silabi hiyo kuwa na ama toni chini au toni juu katika nafasi inamotokea katika neno husika kulingana na dhamira ya mzungumzaji. Pia, utokeaji wa andamio nazali katika neno lenye silabi moja unafanya neno hilo kuwa na toni juu (Nelson, 2013; 2022). Hivyo, usilabishaji wa sauti nazali hautokezi katika umbo la nje la neno husika lenye kilele cha silabi, yaani irabu.

## 2.3 Muundo wa Silabi

Kama ilivyo katika lugha nyingi za Kibantu, silabi katika Kimochi ina miundo mbalimbali ambayo hupangika kutegemea aina ya Konsonanti na irabu zinavyofuatana.Turejelee data ifuatayo katika Data Na.2, ambapo alama *$* ina maana ya mpaka wa silabi:

(2).

a. I, Irabu pekee, kwa mfano, $***u***$***ó***$***u$*** -"woga" $ ***u***$***a***$*ngá*$*ri$*- "kiu"$

*u*$*í*$*wi* -“wizi”

b. K, Konsonanti (nazali) pekee, kwa mfano, ***m***$*ká*$*pe* –“mpige” ***n***$*ndé*$***ny*** -“twendeni”
c. KI, kwa mfano, *i*- $***wa***$***ta***$***rá***$***ma*** -“kuwasaidia”, *i-**fi***$***hí***$***r̲a*** -“ku- lia”
d. KII, kwa mfano, ***í***- $***daa$***- “ku-nuka”, **í**- $***laa$*** - “ku-lala”
e. KKI, kwa mfano, *i-da*$***pfú***$*na* -“ku- tafuna”, *i-se*$***mbe***$*r̲i*$*á*$*na* - “ku-sogezeana”
f. KKKI, kwa mfano, *i*- *$o$**ndza*** -“kunyonyesha”
g. KYI, kwa mfano, *$ko$m$**kya*** **“** kumekucha” *i-$fi$hi$**ryo$*** “kuliliwa”
h. YI, kwa mfano, *i*- *$**wa*** - “kuiba”, i- *$ko$**ya*** - “kukuta”
i. KY, kwa mfano, $*ku$nde$**ny*** - “pendeni”, *i-$le$ke$**ny*** – “iacheni”

Hivyo katika data (2), tunaona miundo mbalimbali ya silabi na jinsi inavyoumbika katika maneno ya Kimochi.

## 2.4 Michakato ya Kifonolojia

Katika Kimochi kuna baadhi ya michakato ya kifonolojia ambayo pia huathiri maumbo ya nomino na vitenzi. Michakato hiyo huonesha kuathiriana kwa sauti ama zilizo jirani au zilizo mbali kimfuatano. Sauti hizo zaweza kuathiriana irabu kwa irabu, konsonanti kwa konsonanti au irabu na konsonanti. Ifuatayo ni baadhi ya michakato hiyo na jinsi inavyojitokeza katika lugha ya Kimochi.

### 2.4.1 Uyeyushaji

Uyeyushaji ni mchakato wa kifonolojia unaogeuza irabu kuwa kiyeyusho pale ambapo irabu za juu mbele /i/ na nyuma /u/ zinapokuwa zimepakana na silabi nyingine zinazoanza na irabu nyingine tofauti baada ya mpaka wa silabi; Irabu /i/ huwa [j] na /u/ huwa [w]. Tuangalie data ifuatayo katika (3)

| | | | |
|---|---|---|---|
| (3) | */ku+ipfo/* | → *[kwipfo]* | kuna … |
| | */ki+umu/* | → *[kyumu ]* | kigumu |
| | */kahalu+o/* | → *[kahalwo]* | kajibu |
| | */ki+awo/* | → *[kyawo]* | cha kwao |
| | */ki+ela/* | → *[kyela]* | chakula |

Katika (3), tunaona kwamba irabu /i/ huyeyuka na kuwa [j] inapofuatana na irabu yoyote katika mpaka wa irabu isipokuwa yenyewe, wakati irabu /u/ huyeyuka na kuwa [w] inapofuatwa na irabu yoyote katika mpaka wa irabu isipokuwa yenyewe. Ufafanuzi huu waweza kuelezwa kwa kanuni isiyo rasmi kama ifuatavyo katika (1):

**Kanuni Na. 1: Uyeyushaji wa Irabu**

a. /u/ → [w] /
b. /i/ → [j] /

Kanuni Na. 1(a) inasema kuwa irabu /u/ ya juu nyuma inabadilika kuwa kiyeyusho cha midomo [w] katika mazingira ya kufuatiwa na irabu yoyote katika mpaka wa

silabi isipokuwa ile inayofanana nayo. Kanuni Na. 1 (b) inasema kuwa irabu /i/ ya juu mbele inabadilika kuwa kiyeyusho cha kaakaa gumu [j] katika mazingira ya kufuatiwa na irabu yoyote isipokuwa ile inayofanana nayo.

### 2.4.2 Muungano wa Sauti

Ni mchakato ambao sauti mbili zinazopakana katika mpaka wa silabi huathiriana. Muungano wa sauti huweza kutoa athari za namna mbili. Kwanza sauti zote mbili zilizoathiriana huweza kubakia lakini hakuna hata moja inayobaki na sifa zake zote pasi na kupunguza au kuongeza kitu chochote. Athari nyingine ni vitamkwa vyote viwili huungana na kutoa kitamkwa kimoja ambacho ni tofauti na vitamkwa hivyo viwili, athari hii inajitokeza katika Kimochi. Wakati mwingine muungano wa sauti huweza kuzalisha sauti ambayo wakaa wake huongezeka na kuwa mrefu, hivyo kuwa irabu ndefu au konsonanti ambatani (taz. Massamba na wenzie (2004), Massamba (2004; 2010; 2011)). Katika Kimochi, kuna mchakato wa kifonolojia wa muungano wa sauti kama inavyoonekana katika Data Na. 4:

(4) a. a+i → e: → /*waícha/* → /*wé:cha/* → wanakuja,
- /*alékáíhénda*/ → /*aléké:hénda*/ → huwa haendi
- /*wam**áí**énde*/ wameileta → [*waméénde*] wameleta
- /*n**aí**cha*/ anakuja → [*né:cha?*] anakuja?

b. u+a → o: → wuáhwa → wo:ho → kuuwawa
- /*naléw**úá**hwa*/ aliuliwa → [*naléwó:ho*] aliuwawa

c. u+e → o: → sue → so: → sisi

Katika Data Na. 4 tunaona kuwa muungano wa sauti unatokea pale sauti za irabu zinazototofautiana zinapokutana katika mpaka wa silabi, zinaungana na kuzaa sauti ya irabu tofauti za ama irabu fupi au ndefu. Sauti za irabu zinazotokea baada ya muungano wa sauti zinazobadilika na kuwa sauti ya irabu nyingine kabisa. Pia, tunaona kuwa kuna mabadiliko ya umbo la neno na fonolojia ya neno inayotokana na muungano wa sauti ambao unaathari katika wakaa wa irabu, yaani kuwa irabu ndefu au irabu fupi, msuko wa idadi ya vitamkwa na ruwaza ya toni ya neno husika.

Kanuni ya kifonolojia inayosharabu Data Na. 4 ni kama inavyoonekana katika Kanuni Na. 2:

**Kanuni Na. 2: Muungano wa sauti za irabu**

a. /a + i/ → [e]
b. /a + i/ → [e:]
c. /u + a/ → [o:]
d. /u + e/ → [o:]

Katika kanuni (2), tunaona kuwa muungano wa irabu /a + i/ unatoa matokeo mawili yenye tofauti ya wakaa. Matokeo hayo ni ya sauti [e] ambayo ni irabu fupi na [e:] ambayo ni irabu ndefu. Matokeo haya ya tofauti ya wakaa wa irabu yanategemea

mazingira ya irabu zinazoungana katika neno husika. Wakati mwingine muungano wa sauti unaweza kutoa matokeo yenye kufidia wakaa katika neno husika kama inavyoonekana katika kanuni (b). Vilevile, tunaona kuwa muungano wa irabu /u + a/ na /u + e/ unatoa matokeo ya kufanana yenye sauti ya irabu ndefu [o:] yenye kufidia wakaa katika neno husika kama inavyoonekana katika kanuni (c) na (d). Matokeo haya yanaathiri mofolojia ya neno kwa kupunguza vitamkwa lakini hayaathiri ruwaza ya toni kwa sababu kuna ufidiaji wa wakaa.

Aidha, katika Kimochi kuna muungano wa sauti za konsonanti. Kuungana kwa silabi za sauti nazali za midomo /mu/ inapopakana na mzizi wa kitenzi unaoanzia na kiyeyusho cha midomo [w], huzaa sauti /mb/ kwa kuwa /mu/ hudondosha irabu /u/ na kulazimisha [w] ifanane na nazali za midomo, hivyo, kubadilika na kuwa kizuio [b] na wakati huohuo sauti /m/ hufidia wakaa wake na kuwa konsonanti ambatani /ṁ/ yenye kumaanisha sauti /mm/.

**Kanuni Na. 3: Muungano wa sauti za konsonanti**

/mu/ → [ṁb:] / − $ /w/

Kanuni inaeleza kuwa /mu/ inabadilika kuwa [ṁb:] katika mazingira ya kufuatiwa na /w/ katika mpaka wa silabi.

Mchakato wa muungano wa sauti za konsonanti unaathiri ruwaza ya vipambasauti kwa sababu usilabi wa sauti nazali unaofinyangwa katika andamio nazali na kupunguza kwa idadi ya silabi katika neno. Tuangalie data (5):

(5)

a. / *i-muwésa/ → [iṁbésa]* kumuuliza
b. */i-muwáha/ → [iṁbáha]* kumuua
c. */i-muwíkía/ → [iṁbíkía]* kumjengea
d. */i-muwíhíṟía/ → [iṁbíhíṟía]* kumrudishia

Tukiangalia kwa makini Data Na. 5(a) na (b), tunaona kuwa kuna ruwaza ya kipambasauti toni ya chini-chini-juu-chini (CCJC) katika umbondani na chini-juu-chini (CJC) katika umbonje. Mfano (c) una ruwaza ya toni ya CCJJC katika umbondani na chini-juu-juu-chini (CJJC) katika umbonje. Pia, data (d) kuna ruwaza ya toni chini-chini-juu-juu-juu-chini (CCJJJC) katika umbondani na CJJJC katika umbonje. Kiujumla, tunaona kuwa mchakato wa muungano wa sauti za konsonanti unasababisha udondoshaji wa C ya kushoto katika umbonje la neno husika kutokana na kupungua kwa idadi ya silabi.

### 2.4.3 Udondoshaji sauti

Baadhi ya vitamkwa vinavyounda vitenzi vya Kimochi vina mchakato wa kimofofonolojia wa udondoshaji wa sauti kama inavyoonekana katika data (6):

(6).

a) /*nal**éí**énde*/ aliileta → [*naléénde*] alileta
b) /*no**í**énde*/ umeileta → [*no**é**nde*] umeleta

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| c) | /*ny**ió**kéámbúya*/ | huwa unaangalia | → [*nyo:kéámbúya*] | huangalia |
| d) | /*ulákús**úo***/ | usikasirike | → [*ulákúsó*] | usikasirike |
| e) | /*w**aé**kékaa*/ | huwa wanakaa | → [*we:kékaa/* | hukaa |
| f) | /*w**aó**se/* | wote | → [wó:se] | wote |

Katika Data Na. 6 tunaona kuwa kuna udondoshaji wa sauti /i/ ambayo ni kiambishi cha yambwa katika Data Na. 6 (a – c). Udondoshaji wa sauti /u/ ambayo ni irabu ya shina la neno *suo* "kasirika", unaonekana katika Data Na. 6 (d). Pia, kuna udondoshaji wa sauti /a/ ambayo ni sehemu ya kiambishi cha ngeli katika data 6 (e – f). Udondoshaji wa sauti unatokea pale sauti za irabu zinazotofautiana zinapokuwa zinakutana katika mpaka wa silabi. Sauti ya irabu inayobakia baada ya udondoshaji wa sauti hutokea katika mojawapo ya sauti za irabu zilizokutana katika mpaka wa irabu.

Katika udondoshaji wa sauti tunaona kuwa kuna mabadiliko ya umbo la neno na toni ya neno inayotokana na udondoshaji wa sauti ambao unaathari katika wakaa wa irabu katika mfano (a), tofauti ya msuko wa idadi ya vitamkwa baada ya udondoshaji unajitokeza katika mfano wa 6 (a-f) na ruwaza ya toni ya silabi za neno husika mfano wa 6 (a-f) kama inavyoonekana katika data za kielelezo cha udondoshaji wa sauti za irabu. Mchakato huo wa kifonolojia waweza kutengenezewa kanuni ya mchakato wa Kifonolojia kama ifuatavyo:

**Kanuni Na. 4: Udondoshaji wa Sauti za Irabu**

a) /e + i/ → [e]
b) /i + e/ → [e]
c) /i+o/ → [o:]
d) /u + o/ → [o]
e) /a+e/ → [e:]
f) /a+o/ → [o:]

Katika kanuni ya udondoshaji wa sauti tunaona kuwa sauti /i/ ambayo ni kiambishi cha yambwa inadondoka pale inapokutana na sauti /e, o/ katika mpaka wa silabi. Sauti /u/ ambayo ni sehemu ya shina la neno inadondoka pale inapokutana na sauti /o/ katika mpaka wa silabi. Sauti /a/ ambayo ni sehemu ya kiambishi ngeli inadondoka pale inapokutana na sauti /e, o/.

Aidha, wazungumzaji wa lugha ya Kimochi hudondosha irabu /i/ inapokuwa imetanguliwa na nazali ya kaakaa gumu [ň] hasa pale inapojitokeza mwishoni mwa neno husika katika kategoria tofauti. Sauti hiyo hudondoshwa ama hufifishwa katika utamkaji wake lakini likitamkwa neno husika polepole sauti hiyo husikika kwa uwazi.. Tuangalie data ifuatayo katika 7:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (7). | a. | *ambuyeny* | angalieni |
| | b. | *adanyieny* | sikilizeni |
| | c. | *amony* | peke yake |

| | | |
|---|---|---|
| d. | *sieny* | furahani |

Vilevile, kuna udondoshaji changamani wa sauti za irabu, konsonanti na silabi katika baadhi ya vitenzi katika Kimochi. Kuna udondoshaji wa sauti mwanzoni, kati na hata mwishoni mwa neno husika. Kama udondoshaji kati wa silabi umetokea, basi neno husika hupunguza sauti pasi athari ya maana na mijongeo ya baadhi ya vipambasauti. Udondoshaji wa sauti unapotokea katika neno na kubakia na silabi inayoishia na irabu, basi kunatokea urefushaji irabu wa ufidiaji wakaa ingawa ufidiaji huo hauwezi kulingana na wakaa uliokuwapo hapo awali (taz. Massamba, 2011). Wakati mwingine udondoshaji hujitokeza katika uimbaji unaotokana na ujuzi wa lugha wa ukamilishaji wa mizani ili kupata mapigo ya kimuziki yanayohitajika. Sauti za irabu, konsonanti na silabi zinazodondoshwa zimekolezewa wino (taz. Kitabu cha nyimbo za Kikristo kwa lugha ya Kimochi kiitwacho Kitabu *kya Siri* (1986) na Biblia iitwayo *Mkundana Mhya* (1998)). Tuchunguze Data Na.8 kama ifuatavyoifuatayo :

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (8) a. | *e**chí**kúda* | → | *ekúda* | atakuacha |
| b. | *ne**chí**kúhálúkía* | → | *ekúhálúkía* | atakugeukia |
| c. | *ngamá**rís**a* | → | *ngamáá* | nimemaliza |
| d. | ***n**ahó**mb**ó**ka*** | → | *nyahóó* | ameanguka |
| e. | ***n**omáshí**ka*** | → | *ońshíka* | umeshafika |
| f. | ***n**akúkúnda* | → | *akúkúnda* | anakupenda |
| g. | ***n**ekí**r̲a* | → | *ekír̲a* | ataponya |
| h. | *ochí**nji**rútsa* | → | *ochíńrútsa* | utanifufua |
| i. | *an**jí**láha* | → | *ańláha* | ananiita |
| j. | *am**á**rúka* | → | *aḿrúka* | amefufuka |
| k. | *seh**í**ya* | → | *sehyá* | pisha |

Katika mfano wa 8 (a – k) tunaona kuwa udondoshaji kati wa sauti katika Kimochi ni changamani. Pia, ni vigumu kuuelezea kikanuni mchakato wa udondoshaji wa sauti zilizoanishwa kwa sababu hakuna kanuni maalumu inayoongoza baadhi ya udondoshaji kati wa irabu, konsonanti na silabi. Kinachoonekana ni ukatishaji wa maneno usioathiri maana iliyokusudiwa katika taarifa inayotolewa. Ukatishaji huo wa maneno hutegemea sana umahiri wa lugha wa mzungumzaji.

### 2.4.4 Mabadiliko ya Sauti

Lugha ya Kimochi ina sifa za kifonolojia ambapo viambishi awali vya idadi vya nomino hubadilika kutoka kwenye umoja na kwenda kwenye wingi. Tuchunguze Data Na. 9 kama ifuatavyo:

| 9. | **Umoja** | | **Wingi** | |
|---|---|---|---|---|
| a. | *okókúo* | kiwiko | *ngókúo* | viwiko |
| b. | *olóríka* | kigoda | *njolóríka* | vigoda |
| c. | *orúsu* | uzi | *ndúsu* | nyuzi |
| d. | *óchaa* | ukucha | *njáá* | kucha |

Katika Data Na. 9 (a) – (d) tunabaini kuwa katika Kimochi kuna mchakato wa kifonolojia wa mabadiliko ya viambishi awali vya idadi kutoka umoja kwenda wingi na mabadiliko ya sauti za viambishi awali yanatokea katika mahali pamoja pa matamshi. Tukichunguza mfano wa 9 (a) *okókúo* "kiwiko" katika umoja na kuwa *ngókúo* " viwiko" katika wingi kuna mabadiliko ya sauti ya irabu [o] inapopakana na konsonanti /k-/ katika mpaka wa silabi, inabadilika na kuwa sauti nazali /n-**/** yenye umbo la andamio nazali **/**ng-**/**. Tufahamu kuwa sauti konsonanti, kipasuo, sighuna [k] na andamio nazali /ŋg/ zinatamkiwa katika mahali pamoja pa matamshi ambapo ni katika kaakaa laini.

Katika Data Na. 9 (b) /*olóríka/* "kigoda" katika umoja na /*njolóríka/* "vigoda" katika wingi na (d) *óchaa* "ukucha" katika umoja na *njáá* "kucha" katika wingi inaonesha kuwa sauti irabu /o/ inapopakana na konsonanti ambayo kipasuo, si ghuna /č/ au kilainisho /l/ katika mpaka wa silabi inabadilika na kuwa sauti nazali yenye umbo la andamio nazali /nj/ ambapo sauti /c/ na /l/ hutamkiwa katika mahali pamoja pa matamshi ambapo ni kaakaa gumu.

Katika Data Na. 9 (c) /*orúsu/* "uzi" katika umoja na /*ndúsu/* "nyuzi" katika wingi tunaona kwamba sauti irabu /o/ inapopakana na konsonanti ambayo ni kilainisho /r/ katika mpaka wa silabi inabadilika na kuwa nazali yenye umbo la andamio nazali /nd/ ambapo sauti /r/ na /nd/ hutamkiwa katika mahali pamoja pa matamshi ambapo ni katika ufizi.

Hivyo, mabadiliko ya kifonolojia ya viambishi awali vilivyobainishwa katika Kimochi, yanatupa taarifa ya jumla kuwa sauti irabu /o/ inapokutana na konsonanti halisi katika mpaka wa silabi ($) inabadilika na kuwa sauti nazali yenye umbo la andamio nazali zinazotamkiwa katika mahali pamoja pa matamshi. Aidha, katika Kimochi sauti nazali ya /n-/ inajitokeza katika alomofu **{**n-, ng-, nj-, m-, mb-, nd, ṅ, na ṁ**}.** Kwa hiyo, mabadiliko ya kifonolojia ya viambishi awali vilivyobainishwa katika Kimochi yanaweza kuundiwa kanuni ya kifonolojia kama inavyoonekana katika Kanuni Na. 5:

**Kanuni Na. 5: Mabadiliko ya Sauti**

$$o \longrightarrow \begin{bmatrix} \text{ŋg} \\ \text{nd} \\ \text{nj} \end{bmatrix} \Big/ __ + \$ \begin{bmatrix} \text{k} \\ \text{r} \\ \left.\begin{matrix} \text{l} \\ \check{\text{c}} \end{matrix}\right\} \end{bmatrix}$$

Kanuni ya mabadiliko ya sauti za baadhi viambishi vya idadi katika nomino za Kimochi inaeleza kuwa sauti irabu /o/ inabadilika kuwa sauti nazali /ŋg/ katika mazingira ya kufuatiwa na sauti konsonanti /k/ kwenye mpaka wa silabi. Pia, sauti irabu /o/ inabadilika kuwa sauti nazali /nd/ katika mazingira ya kufuatiwa na sauti

konsonanti /r/ kwenye mpaka wa silabi. Vilevile sauti irabu /o/ inabadilika kuwa sauti nazali /nj/ katika mazingira ya kufuatiwa na konsonanti ama /l/, au /č/ kwenye mpaka wa silabi. Kwa kifupi tunaweza kusema kuwa sauti irabu /o/ inabadilika na kuwa sauti nazali katika umbo la andamio nazali [ŋg, nd, nj] katika mazingira ya kufuatiwa na sauti za konsonanti halisi [k], [r] [l ] na [č] mtawalia kwenye mpaka wa silabi.

**3.0 Hitimisho**

Katika makala haya tumeonesha baadhi ya vipengele vya kifonolojia kama vile irabu, konsonanti, muundo wa silabi, na michakato ya kifonolojia. Katika idadi ya konsonati na irabu, tumeona kwamba Kimochi kina idadi sawa za sauti hizo kama ilivyo katika lugha nyingine za kibantu. Katika muundo wa silabi, tumeonesha kwamba Kimochi kina aina mbalimbali za miundo ya silabi wakati michakato ya kifonolojia, tumeonesha kwamba, michakato hiyo hujitokeza katika mpaka wa silabi. Kwa ujumla wake, masuala ya fonolojia ya vipande sauti huru vilivyojadiliwa ni majumui, yanajitokeza pia katika lugha za kibantu.

**Marejeleo**


Chomsky, N and M. Halle, (1968) *The Sound Pattern of English*. New York, Larper and Row.

Ismail, J.H. (2011) *A Tonological Study of Meeto-Makua of Southern Tanzania.* Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

K.K.K.T. (1986) *Kitabu kya Siri: Mochi-Mbokomu*. Tanzania. Vuga Press.

K.K.K.T. (1998) *Mkundana Mhya: Mdedie fo Kimochi*. Dodoma: The Bible Society of Tanzania.

Massamba, D.P.B. (2004) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2005) ‘‘The Role of Supresegmental Phenomena in the Analysis of Bantu Languages: With Special Reference to Ciruuri’’. Katika LOT *Ocassional Papers in Linguistics*, Dar es Salaam, LOT Publications, Juz. 1. kur. 88-105.

Massamba, D.P.B. (2011) *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2010) *Phonological Theory: History and Development* (Revised Edition), Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M. na Msanjila, Y.P. (2004) *Fonolojia ya Kiswahili: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

MLUTA. (2009) *Atlasi ya Lugha za Tanzania*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mrikaria, G. (2008) *KIMOCHI; Msamiati wa Kimochi-Kiswahili-Kiingereza.* University of Dar es Salaam, Languages of Tanzania (LOT) Project Publications.

Nelson, C. (2013) *Toni katika Vitenzi vya Kimochi*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salam.

Nelson, C. (2022). *Ruwaza za Toni za Kisarufi katika Kimochi*. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Polome, S.A (1971) *Phonological Survey of the Chaga Dialect of Tanzania*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Austin Texas.

Raum. J. (1909/1964) *Versuch einer Grammatik der Dschaggasprache (Moschi-Dialekt).* U.S.A: The Gress Press Incorporated.

Sloat, C., Taylor, H.S., na Hoard, J. E. (1978) *Introduction to Phonology*. *New Jersey,* U.K: Prentice-Hall, Inc.

TUKI. (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

TUKI. (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Oxford University Press.